OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA.

Shule ya Sekondari Nkende,
S.L.P 325,
TARIME.

14/12/2020.

Kumb. Na.TRM/NKD/SS/J.I/18.

Jina la Mwanafunzi.....
S.L.P.....,
TARIME.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NKENDE HALMASHAURI YA MJI WA TARIME MKOA WA MARA MWAKA -2021.

1. UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule hii mwaka 2021.**HONGERA SANA**.

Shule ya Sekondari Nkende ipo umbali wa kilometa 2.5 toka mjini. Shule hii ni ya kutwa iko eneo la mtaa wa **KINYAMBI**, Kata ya Nkende, barabara kuu iendayo **SIRARI – MUSOMA**. Shule hii ni ya mchanganyiko wa wasichana na wavulana.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe 11/01/2021 unatakiwa kuripoti shuleni Tarehe 11/01/2021.Kila mwanafunzi aje na mzazi/mlezi wake saa 2:00 asubuhi kwa **USAJIL** I. Mahitaji na vifaa vyote vya shule vitakaguliwa siku ya kuripoti.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

a) Wavulana

i. Suruali mbili zenye mifuko mitatu, Marinda mawili kila upande na zisizo na madoido (Moja **NYEUSI** na ya pili **DARK BLUE**) (**zisiwe katika mtindo wa kata K au Model).** Upana chini **usipungue sentimeta 18** na iwe na pindo (turn up) kitambaa ni **ISTIM namba moja.**

ii. Shati nyeupe mbili mikono mifupi Tetron. (**Zisiwe zinabana mwili).**

iii. Viatu vya ngozi NYEUSI vya kamba visivyo na madoido yoyote yale.(SIYO RABA)

iv. Soksi nyeupe jozi mbili ndefu.

v. Sweta moja rangi ya bluu.

vi. T- Shirt ya shule. (Utaratibu wake utatolewa shuleni).

b) **Wasichana.**

i. Sketi mbili zenye marinda na urefu wa kufunika magoti (**cm 12 kutoka kwenye magoti kwenda chini)** upana wa pindo la tumboni uwe inchi mbili au mbili na nusu, moja nyeusi yenye mchirizi wa kijani na nyingine ya BLUU BAHARI yenye mchirizi mweupe. "**SKETI ZOTE ZIWE ZA KITAMBAA KIZITO**" (**TUNASISITIZA ZISIWE FUPI**) Kitambaa ni **ISTIM namba moja.**

ii. Shati nyupe mbili za mikono mifupi Tetron. (**zisiwe zinazobana mwili)**

iii. Viatu vya ngozi **NYEUSI** vya kamba visivyo na madoido yoyote yale vyenye kisigino kifupi. (SIYO RABA).

iv. Soksi ndefu nyeupe (stocking) jozi mbili.

v. Sweta moja rangi ya bluu.

vi. T- Shirt ya shule (Utaratibu wake utatolewa shuleni).

Tanbihi: Wanafunzi wasichana wa **KIISLAM** watavaa sketi zenye marinda ndefu zinazofunika miguu, shati (blauzi) nyeupe mikono mirefu na kitambaa cha kichwa (Hijabu) rangi nyeupe isiyo na urembo wowote.

c) Sare ya michezo kwa shule hii ni **tracksuit ya rangi ya bluu bahari (light blue)** kwa wavulana na wasichana, isiwe inayobana mwili. Kila mwanafunzi anatakiwa kuwa na viatu (raba) vya michezo.

2.2. MAHITAJI YA VIFAA.

(1). Mathematical set moja.
(2). Madaftari makubwa – counter book Quire 2 yawe kumi na moja.
(3). Begi dogo la vifaa. USINUNUE MIFUKO YA NYLON "PEPSI", wala mifuko ya Bob marley.
(4). Picha nne (4) za rangi (**stamp size)**
(5). File moja aina ya "spring file" (isiyo ya plastic) ya rangi ya blue.

3. **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na chini ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na Uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.

d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
e) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
f) Kuvaa sare za shule wakati wote unapotakiwa.
g) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wowote na
h) Kutunza Mali za umma.

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Kuwa mjamzito/ kupata mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kuwa na simu ya mkononi.

1.0. MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

1) Fomu ya maelezo ya uchaguzi wa Daktari kuhusu afya ya mwanafunzi. Fomu hii ijazwe na Daktari/ Mganga wa Hospitali ya Wilaya ya Serikali baada ya kupimwa mwanafunzi.
2) Fomu ya URAIA leta Photocopy ya cheti cha kuzaliwa au jaza AFFIDAVIT FORM toka ofisi ya Mkuu wa Wilaya.
3) Fomu ya maelekezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.

4) Fomu ya mzazi/mlezi kukiri kukubaliana na sheria za shule, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

5) **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

KARIBUNI SANA NKENDE SEKONDARI.

.....

MKUU WA SHULE.

SHULE YA SEKONDARI NKENDE
FOMU YA MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI NA MZAZI/MLEZI.
KUKUBALIANA NA SHERIA ZA SHULE.

2. **TAARIFA ZA MWANAFUNZ**I
   a) Jina kamili la Mwanafunzi.....
   b) Tarehe ya kuzaliwa.....
   c) Mahali anapoishi (Mtaa/Kata).....
   d) Uraia; MTANZANIA/SI MTANZANIA.....
   e) Shule aliyotoka .....

3. **TAARIFA ZA MZAZI/MLEZI**.
   a) Jina la Mzazi/Mlezi.....
   b) Kazi ya Mzazi/Mlezi .....
   c) Anuani ya Mzazi/Mlezi .....
   d) Mahali anapoishi (Mtaa/Kata).....
   e) Namba ya simu.....
   f) Ndugu/Jamaa wa karibu wa Mwanafunzi. (Jaza jedwali lifuatalo).

Na	Jina la ndugu/ Jamaa	anapoishi	uhusiano	Namba ya simu

4. **AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI**

Mimi .....nimesoma na kuyaelewa maelekezo yote ya kujiunga na shule ya Sekondari Nkende na nimekubali kuipokea nafasi niliyopewa. Ninaahidi kufuata maelekezo yote, sheria na taratibu za shule. Sitashiriki wala kujihusisha na migomo, fujo wala makosa ya jinai. Endapo nitakiuka

kiapo hiki uongozi wa shule uchukue hatua za kinidhamu dhidi yangu.

Sahihi ..... Tarehe .....

5. AHADI YA MZAZI/ MLEZI.

Mimi .....mzazi/mlezi wa mwanafunzi ninakiri kukubaliana na sheria za shule, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule, niko tayari kupokea uamuzi utakaotolewa na shule endapo mwanafunzi atavunja sheria, kanuni na taratibu za shule. Pia ninaahidi kushirikiana kwa karibu na uongozi wa shule katika malezi ya mwanangu muda wote wa masomo yake ikiwa ni pamoja na kufuatilia maendeleo yake kitaaluma. Nitampatia mahitaji yote muhimu kama uongozi wa shule utakavyokuwa ukielekeza.

Sahihi ..... Tarehe .....

Fomu hii itasainiwa siku ya mwanafunzi kuripoti shuleni.

KIAMBATANISHO "B"

MINISTRY OF EDUCATION AND VOCATIONAL TRAINING.

MEDICAL EXAMINATION FORM.

Full Name .....

Age .....Height (In Cms) .....Weight.....

1. Blood court (Red and White).....
2. Stool Examination.....
3. Urine Analysis.....
4. Syphilis and other V.D.....
5. T.B and Leprosy Test.....
6. Eye Test.....
7. Ears Test.....
8. Chest Test.....
9. Abdominal Test.....
10. Plano Test (Girls).....
11. Spleen.....

Additional Information E.g Physical Defects of Impairments Infection Chronic or Family Disease (e.g. Sickle cell) Inability to Eat certain foods Etc.

.....
.....
.....
.....

.....
.....
.....
.....
.....
.....

I certify that the above named student is Fit/Unfit to pursue Secondary Education as Started above.

Signature .....
Designation .....
Station .....
Date .....